# Tozo zinazokwamisha ukuaji wa mazao ya mifugo, uvuvi kuondolewa

Simiyu
Na MWANDISHI WETU

SERIKALI imesema inatafuta namna ya kuwa na kituo kimoja cha kulipia tozo zote za mazao ya mifugo na uvuvi, pamoja na kuondoa tozo ambazo zinakwamisha sekta hizo zisikue.

Akizungumza juzi na baadhi ya wavuvi katika Kata ya Nyamikoma, iliyopo Wilaya ya Busega, mkoani Simiyu, wakati wa ziara yake ya siku moja mkoani humo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema wizara itaangalia tozo ambazo zitakuwa rafiki kwa wawekezaji, wafanyabiashara pamoja na wafugaji na wavuvi wa hali ya chini, ili kuhakikisha sekta za mifugo na uvuvi zinachangia kwa sehemu kubwa pato la taifa.

"Tutaenda kuangalia ni tozo zipi na baadhi tayari mmeshazitaja, zikiwemo za kusafirisha mazao ya mifugo na uvuvi nje ya nchi, halafu tunatafuta namna ya kuwa na kituo kimoja cha kulipia hizi tozo zote," alisema Ndaki.

Waziri Ndaki ambaye amefuatana na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Pauline Gekul, ameongeza kuwa uwepo wa tozo ambazo zitakuwa rafiki katika kukuza sekta za mifugo na uvuvi kutasababisha watu wengi kuwekeza katika sekta hizo na kuongeza pato la taifa kwa kuwa shughuli za kuchumi zitaongezeka.

Kwa upande wake, Gekul ameendelea kusisitiza kuwa watu wanaondelea kujihusisha na uvuvi haramu kuacha mara moja vitendo hivyo kwa kuwa wizara haitafumbia macho watu ambao hawataki kuacha kuharibu mazao ya uvuvi kupitia vitendo hivyo.

Amesema ni wakati sasa jamii kushirikiana na serikali kuwabaini watu wanaojihusisha na uvuvi haramu kwa kuwa wanaishi katika maeneo wanayofahamika, ili serikali ichukue hatua na kwamba wizara itaendelea kutoa elimu juu ya athari ya uvuvi haramu kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Siku moja kabla ya kuanza ziara ya kikazi mkoani Simiyu, Ndaki wakati akihitimisha ziara ya siku mbili mkoani Mwanza aliefika katika Kijiji cha Kitongosima kilichopo Wilaya ya Magu, mkoani humo na kuzungumza na jamii ya wavuvi na kuwasisitiza waanze kufuga samaki kupitia njia za vizimba na mabwawa, ili kujiongezea kipato na kuongeza kuwa mahitaji ya soko la samaki kwa sasa ni kubwa.

Mhe. Ndaki alimwagiza Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, kuhakikisha anaanzisha utaratibu wa kuwepo kwa kizimba cha mafunzo kwa ajili ya kufugia samaki na kuhakikisha wataalamu kutoka wizarani wanafika katika kijiji hicho kuwafundisha wananchi namna ya kufuga na kulisha samaki, ili jamii ya hapo iweze kupata mapato kupitia mazao ya uvuvi.

Scanned with CamScanner

# Wafugaji watakiwa kuogesha mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

WAFUGAJI wameshauriwa kuogesha mifugo yao ili kupambana na magonjwa na kuondoa kizuizi kwa nchi kuuza nyama nje kutokana na viwanda vya kuchinja mifugo na kuchakata nyama kutopata mifugo bora.

Akizungumza katika kijiji cha Kinango, wilaya ya Magu, mkoani Mwanza jana wakati akishuhudia uogeshaji mifugo ili kudhibiti magonjwa mbalimbali, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema mifugo mingi ikiwamo ng'ombe ikitunzwa vizuri inaweza kuingiza fedha nyingi ikiwamo za kigeni.

"Mifugo iogeshwe kwa kufuata taratibu na utaalamu ili kuiongezea nyama ubora."

"Nchi yetu tuna ng'ombe wengi sana lakini wengi siyo bora kama inavyotakiwa sasa tunatakiwa kutoka kuwa na ng'ombe wengi tu bali tuwe na ng'ombe walio bora."



"Tukiwa na ng'ombe wengi wasio bora hawatusaidii sana katika maisha yetu kwa sababu lengo la kuwa na ng'ombe ni ili atupe nyama, maziwa na kipato sasa tufikirie kuwa na ng'ombe bora na moja ya njia ya kuwa na ng'ombe bora ni hii ya kuwaogesha," alisema.

Ndaki akiwa ameambatana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul katika ziara hiyo alisema njia nyingine ya kuwa na ng'ombe bora ni wafugaji kuhakikisha mifugo yao inapata malisho bora.

Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania (TMB), Iman Sichalwe aliwaeleza wafugaji kuwa kuogesha mifugo kudhibiti magonjwa ni muhimu kwani unaboresha afya ya mfugo ikiwamo nyama na ngozi hivyo kuvifanya viwanda kupata malighafi nzuri na kuwaongezea vipato wananchi kwa kupata masoko ya kuuza mifugo yao.

"Serikali pia itapata fedha kupitia tozo mbalimbali pamoja na upatikanaji wa fedha za kigeni na hili litawezekana endapo mifugo haitaathiriwa na magonjwa ili kupata nyama bora na kutengeneza bidhaa zitokanazo na ngozi bora," alisema Sichalwe.

Scanned with CamScanner

kuzungumza na wajumbe wa

jumu miundombinu ya TTCL

(TCRA) kufanya utafiti na

ofisini.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kushoto) na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Pauline Gekul wakipatiwa maelezo na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi, Dk Rashid Tamatamah, namna ya kufuga samaki kwa njia ya vizimba wakati waziri huyo alipotembelea Kijiji cha Kitongosima Wilaya ya Magu Mkoani Mwanza, kujionea namna mwekezaji Shamba la Konga anavyofuga samaki kupitia vizimba ndani ya Ziwa Victoria. (Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

Scanned with CamScanner

UVUVI NA UFUGAJI

# Serikali kuanzisha kituo kimoja tozo za mifugo, uvuvi

Johari Shani, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Busega.** Ili kuongeza tija na kumnufaisha zaidi mwananchi, Serikali imesema inaangalia namna ya kuwa na kituo kimoja cha kulipia tozo zote za mazao ya mifugo na uvuvi pamoja na kuziondoa tozo zinazokwamisha maendeleo ya sekta hizo.

Akizungumza juzi na baadhi ya wavuvi wa Kata ya Nyamikoma wilayani hapa, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amesema watazion-doa tozo ambazo si rafiki kwa wawekezaji, wafanyabiashara na wafugaji na wavuvi wadogo ili mchango wa sekta za mifugo na uvuvi uongezeke kwenye pato la Taifa.

"Tutaziangalia tozo zote na baadhi mmeshazitaja zikiwamo za kusafirisha mazao ya mifugo na uvuvi nje ya nchi, na tunatafuta namna ya kuwa na kituo kimoja cha kulipia hizi tozo zote," alisema Ndaki.

**TAARIFA ZAIDI**

**Mchango wa sekta ya mifugo na uvuvi kwenye pato la Taifa ni chini ya asilimia saba hivyo Serikali inaweka mikakati ya kukuza mchango wake kwa kutambua fursa nyingi zilizopo eneo hilo.**

Waziri huyo ambaye alifuatana na naibu wake, Pauline Gekul alisema tozo rafiki zitasaidia kukuza sekta za mifugo na uvuvi kwani watu wengi watashawishika kuwekeza hivyo kuongeza pato la Taifa.

Ahitimisha ziara yake mkoani Mwanza, siku moja kabla hajaanza mkoani Simiyu, Ndaki aliwasisitiza wavuvi kuanza kufuga samaki kwa kutumia mabwawa na vizimba ili kujiongezea kipato. Alitoa ushauri huo alipozungumza na wavuvi wa Kijiji cha Kitongosima kilichopo Wilaya ya Magu.

Alimwagiza katibu mkuu wa uvuvi, Dk Rashid Tamatamah kuhakikisha anaanzisha kizimba cha mafunzo katika kijiji hicho na wataalamu wa wizara wanaenda kuwafundisha namna ya kufuga na kulisha samaki ili jamii inufaike zaidi na mazao ya uvuvi.

Aliagiza hayo baada ya kutembelea vizimba vinavyomilikiwa na Shamba la Konga na kufurahishwa na namna mwekezaji katika kijiji hicho anavyofuga samaki ndani ya Ziwa Victoria.

Kwa upande wake, Gekul aliwaasa kujihusisha na uvuvi haramu kwani wizara haitawafumbia macho.

Scanned with CamScanner

# Tozo zisizo rafiki kukuza sekta ya mifugo na uvuvi kuondolewa

**Na Edward Kondela, Simiyu**

SERIKALI imesema inatafuta namna ya kuwa na kituo kimoja cha kulipia tozo zote za mazao ya mifugo na uvuvi pamoja na kuondoa tozo ambazo zinakwamisha sekta hizo zisikue.

Akizungumza jana na baadhi ya wavuvi katika Kata ya Nyamikoma, iliyopo Wilaya ya Busega Mkoani Simiyu, wakati wa ziara yake ya siku moja mkoani humo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema wizara itaangalia tozo ambazo zitakuwa rafiki kwa wawekezaji, wafanyabiashara pamoja na wafugaji na wavuvi wa hali ya chini ili kuhakikisha sekta za mifugo na uvuvi zinachangia kwa sehemu kubwa pato la taifa.

"Tutaenda kuangalia ni tozo zipi na baadhi tayari mmeshazitaja zikiwemo za kusafirisha mazao ya mifugo na uvuvi nje ya nchi halafu tunatafuta namna ya kuwa na kituo kimoja cha kulipia hizi tozo zote," alisema Ndaki.

Waziri Ndaki ambaye amefuatana na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Pauline Gekul aliongeza kuwa uwepo wa tozo ambazo zitakuwa rafiki katika kukuza sekta za mifugo na uvuvi kutasababisha watu wengi kuwekeza katika sekta hizo na kuongeza pato la taifa kwa kuwa shughuli za kuchumi zitaongezeka.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Pauline Gekul aliendelea kusisitiza kuwa watu wanaondelea kujihusisha na uvuvi haramu kuacha mara moja vitendo hivyo kwa kuwa wizara haitafumbia macho ambao bado hawataki kuacha kuharibu mazao ya uvuvi kupitia vitendo hivyo.

Alisema ni wakati sasa jamii kushirikiana na serikali kuwabaini watu wanaojihusisha na uvuvi haramu kwa kuwa wanaishi katika maeneo wanayofahamika ili serikali ichukue hatua na kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi itazidi kutoa elimu juu ya athari ya uvuvi haramu kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Siku moja kabla ya kuanza ziara ya kikazi Mkoani Simiyu, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki wakati akihitimisha ziara ya siku mbili Mkoani Mwanza amefika katika Kijiji cha Kitongosima kilichopo Wilaya ya Magu mkoani humo na kuzungumza na jamii ya wavuvi na kuwasisitiza waanze kufuga samaki kupitia njia za vizimba na mabwawa ili kujiongezea kipato na kuongeza kuwa mahitaji ya soko la samaki kwa sasa ni makubwa.

Ndaki alimuagiza Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah kuhakikisha anaanzisha utaratibu wa kuwepo kwa kizimba cha mafunzo kwa ajili ya kufugia samaki na kuhakikisha wataalamu kutoka wizarani wanafika katika kijiji hicho kuwafundisha wananchi namna ya kufuga na kulisha samaki ili jamii ya hapo iweze kupata mapato kupitia mazao ya uvuvi.

Waziri Ndaki alibainisha hayo baada ya kutembelea vizimba vya kufugia samaki katika kijiji hicho vinavyomilikiwa na Shamba la Konga na kufurahishwa na namna mwekezaji anavyofuga samaki kwa wingi kwa njia ya vizimba ndani ya Ziwa Victoria kwa kuwa ni sera ya serikali kuhakikisha katika kipindi cha miaka mitano ajira zaidi ya elfu arobaini na tano zinapatikana kupitia ufugaji wa samaki.

Katika kuhakikisha wananchi wa Kijiji cha Kitongosima wananufaika kupitia ufugaji wa samaki Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu Lutengano Mwalwiba aliwataka wanakijiji hao kujiunga katika ushirika ili halmashauri hiyo iweze kuwakopesha fedha kwa ajili ya shughuli za uvuvi.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wafuga Samaki Ziwa Victoria, Cyprian Matembo amemuomba Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki kuangalia namna wizara inavyoweza kuwasaidia kupata vyakula vya samaki kwa bei nafuu kwa kuwa kwa sasa vyakula vingi vimekuwa vikiagizwa kutoka nje ya nchi na kuongeza gharama za uzalishaji.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki jana alihitimisha ziara ya kikazi katika mikoa mitatu ya Kanda ya Ziwa kwenye Mkoa wa Shinyanga, baada ya kufanya ziara kwenye mikoa ya Mwanza na Simiyu, akiambatana na Naibu Waziri wa wizara hiyo Pauline Gekul.



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (wa kwanza kushoto) akifuatiwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Pauline Gekul wakipatiwa maelezo na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Uvuvi, Dkt. Rashid Tamatamah namna ya kufuga samaki kwa njia ya vizimba wakati wa ziara ya kikazi ya Waziri Ndaki katika Kijiji cha Kitongosima kilichopo Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, kujionea namna mwekezaji Shamba la Konga anavyofuga samaki kupitia vizimba ndani ya Ziwa Victoria.** (Picha na Edward Kondela)

# Mradi wa maji Kirando wafikia hatua za mwisho

**Na Mwandishi Wetu, Rukwa**

WANANCHI zaidi ya 7000 wa vijiji vya Kirando na Katete katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa wataanza kupata huduma ya majisafi na salama baada ya siku 60 kuanzia sasa ambapo mradi wa maji wa Kirando ambao umefikia asilimia 85 ya ujenzi kukamilishwa.

Mradi wa maji wa Kirando unatekelezwa na Serikali kwa kutumia wataalam wa Wizara ya Maji kwa utaratibu wa force account kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga (SUWASA) na hadi sasa ujenzi wake umetumia kiasi cha shilingi bilioni 1.5

Mhandisi Anna Kavuruga wa SUWASA akiongea na watendaji wa Mfuko wa Maji alisema kazi ya utekelezaji wa mradi imehusisha pamoja na mengine, ujenzi wa chanzo, ujenzi wa jengo la pampu na kufunga pampu, na ujenzi wa vituo vya kutoa huduma ya majisafi

Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu akimkaribisha Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias Kwandikwa (kushoto) alipowasili katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa akiwa ziarani mkoani humo juzi. (Picha na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tabora)

# Wafugaji watakiwa kuogesha mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

WAFUGAJI wameshauriwa kuogesha mifugo yao ili kupambana na magonjwa na kuondoa kizuizi kwa nchi kuuza nyama nje kutokana na viwanda vya kuchinja mifugo na kuchakata nyama kutopata mifugo bora.

Akizungumza katika kijiji cha Kinango, wilaya ya Magu, mkoani Mwanza jana wakati akishuhudia uogeshaji mifugo ili kudhibiti magonjwa mbalimbali, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema mifugo mingi ikiwamo ng'ombe ikitunzwa vizuri inaweza kuingiza fedha nyingi ikiwamo za kigeni.

"Mifugo iogeshwe kwa kufuata taratibu na utaalamu ili kuiongezea nyama ubora."

"Nchi yetu tuna ng'ombe wengi sana lakini wengi siyo bora kama inavyotakiwa sasa tunatakiwa kutoka kuwa na ng'ombe wengi tu bali tuwe na ng'ombe walio bora."

"Tukiwa na ng'ombe wengi wasio bora hawatusaidii sana katika maisha yetu kwa sababu lengo la kuwa na ng'ombe ni ili atupe nyama, maziwa na kipato sasa tufikirie kuwa na ng'ombe bora na moja ya njia ya kuwa na ng'ombe bora ni hii ya kuwaogesha," alisema.



Ndaki akiwa ameambatana na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul katika ziara hiyo alisema njia nyingine ya kuwa na ng'ombe bora ni wafugaji kuhakikisha mifugo yao inapata malisho bora.

Kaimu Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania (TMB), Iman Sichalwe aliwaeleza wafugaji kuwa 'kuogesha mifugo kudhibiti magonjwa ni muhimu kwani unaboresha afya y[a] mifugo ikiwamo nyama na ngozi hivyo kuvifa[...] viwanda kupata mali[...] nzuri na kuwaongez[...] vipato wananchi kw[...] kupata masoko ya k[...] mifugo yao.

"Serikali pia ita[...] ha kupitia tozo m[...] pamoja na upatik[...] fedha za kigeni [...] awezekana end[...] haitaathiriwa [...] jwa ili kupata [...] na kutengene[...] zitokanazo [...] alisema Sich[...]

# Wanakijiji waomba kujengewa baraba[...]

ha ndipo tupate usafiri wa ... hiyo

Scanned with CamScanner